**SOMO: UWEZESHAJI**

**SEMINA YA WACHUNGAJI NA WAKE ZA WACHUNGAJI WA AICT DAYOSISI YA PWANIILIYOFANYIKA CHUO CHA UJENZI MOROGORO**
**28 NOV - 5 DECEMBER, 2005**
**IMETOLEWA NA MS. R. SHIJA**

**A. UTANGULIZI :**

1. Maombi ya Ufunguzi
2. Shukrani
3. Utambulisho - Mwezeshaji
4. Utambulisho wa Washiriki
    i) Kila Mshiriki ajitambulishe kwa mtindo wa Kumegeana Chapati kutumia kiberiti.
    ii) Washiriki Wajitambulishe kwa Kikundi kwa kuchora picha ya kitu kinachowaunganisha wakitumia Bango.

**MADA : UWEZESHAJI :** Uwezeshaji ni Mbinu Shirikishi inayotumika kuleta Maendeleo ya Watu.

**Maendeleo ni nini?**

Ni Harakati au Mchecheto wa Mtu Binafsi/Kikundi au Jamii ya Watu wanayopitia ili kutoka hali mbaya au hali ya chini ya maisha, kwenda kwenye hali nzuri/ya juu ya maisha . Ni badiliko katika hali ya maisha kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu.

Kwa mfano :

Maendeleo katika hali za Maisha ya Watu/Jamii

| **Hali ya Chini** | **Hali ya Juu** |
|---|---|
| Chakula mlo mmoja kwa siku | Milo mitatu kwa siku. |
| Chakula | Chakula bora |
| Mavazi – yaliyochanika na machafu | Nguo nzuri na safi |
| Maji – machafu hayatoshi | Maji safi & salama ya kutosha, yanapatikana karibu (500M) |
| Afya :<br>Huduma Hosp.Dispensary | Idadi ya wagonjwa kwa Doctor 1<br><br>Umbali mfupi, Dawa ziwepo |
| | |
| | |

Miti shamba, elimu, barabara nk.

Historia ya Harakati za Maendeleo zimepitia hatua kadhaa kabla ya 'Mbinu ya Uwezeshaji' kukubalika kama mbinu sahihi.

**Aina :**

i. **Maendeleo kutoka juu kwenda chini.**

Ni pale Serikali/Wataalam wanapoona kuna mahitaji, wanakuja na kufanya kitu ili kuondoa ile shida katika jamii husika - kwa mfano kuchimba visima vya maji, nk.

**Faida ya Harakati hii :**

Matokeo ya maendeleo huonekana haraka. Inachukua muda mfupi sana kupata matokeo

**Hasara :**

Matokeo haya hayadumu, kwa vile jamii husika wanakiona si kitu chao bali cha Serikali au shirika fulani. Si chao.

**Mfano :**

Kijiji chenye shida ya maji katika nchi moja ya kiislam.
Ngudu - Mwamashimba :
ELEZA ....

ii) **Maendeleo yanayofuata Mahitaji ya Watu:**

Haya yanatokea wakati wa dharura kama Mafuriko/Wakimbizi ili kuokoa maisha ya watu au kupunguza mateso.

iii) **Maendeleo ya Kutoka Chini kwenda Juu (Ushirikishwaji)**

Serikali na Wataalam wanaona hitaji la watu, kisha wana wahusisha wananchi katika maongezi ya namna ya kutatua shida ile wanayoilenga km. Maji, Ujenzi shule nk.

**Faida:**

Mawazo ya wananchi na ujuzi wao unasikilizwa.

**Hasara:**

Matokeo ya mradi yanachukua mrefu kupatikana kutokana na mawasiliano yanayofanyika.

Miradi mingi inachukua harakati hii kwa mfano ujenzi wa mashule MEM - Ingawa wananchi wanahusishwa katika mazungumzo, lakini siyo jamii yote wanaoshiriki, ni wale wenye nafasi na wepesi wa kupokea mambo ndio hushiriki.

**Mfano : Shule wilayani Simanjiro ambapo cement mifuko 100 iliganda na kuharibika.**

Baada ya Harakati zilizotajwa hapo kuonekana kutotoa jibu la kweli juu ya nini mbinu sahihi ya kuleta Maendeleo kwa watu, mtu mmoja Paul Freire alikuja na mbinu mpya **:**

### iv) Mbinu ya Uwezeshaji Maendeleo ya Watu - Paul Freire

Harakati hii Inasisitiza Kumshirikisha na Kumwezasha Mtu au Jamii ya watu kama msingi muhimu katika maendeleo

Paul Freire : Alizaliwa Brazil mwaka 1921 - 1997.- Mwalimu

**Mawazo Yake:**

Aliamini kuwa kila mtu anao uwezo wa kutawala na kujiletea maendeleo ambayo yatabadili hali yake kutoka hali iliyo duni na kuwa na hali nzuri. Paul Freire alitoa philosophy kuwa ili hili litokee mambo yafuatayo lazima yawepo :

- Kutakuwa na Mazungumzo (Dialogue) ya Pamoja.
- Mazungumzo yazingatie elimu na Uzoefu alionao Mshiriki
- Mazungumzo yawe ya Kuheshimiana.(kila mtu apate nafasi ya kusikilizwa kutoa mawazo yake, na mawazo hayo yaheshimiwe.
- Mtu asimwekee mtu mwingine mawazo yake kama ndiyo ukweli.

Paul Freire aliamini kuwa binadamu akipewa nafasi hii basi akili yake inaanza kufunguka na kupata uelewa wa hali yake na mambo yanayomkabili na ni hatua gani anaweza kuchukua.

**Alimwangalia mtu kuwa ana uwezo na upeo mkubwa wa kuweza kutawala maisha yake, isipokuwa kuna mambo ambayo yamemkandamiza mpaka akawa hajiwezi :**

Mwanzo 1: 26 - 31

Mawazo haya yameonekana ni kweli na yanatumika sehemu nyingi duniani.

Hivyo Uwezeshaji ni elimu na mafunzo yatolewayo kupitia Maongezi na Majadiliano ya Mafunzo na Mikakati mbalimbali yanayo mfanya mshiriki kuanza kupata uelewa na utambuzia juu ya :

- Ufahamu kuhusu Hali halisi ya maisha yake,(shida, matatizo, raha)
- Kuwa na Hali ya Matamanio
- Kutambua Mazingira na Rasilmali alizonazo au zinazomzunguka.
- Kutambua Uwezo alionao wa kuweza kutumia rasilmali hizo na
- Namna ya Kupanga Mikakati ya kutumia rasilmali hizo kuondoa shida.
- Kutekeleza Mikakati aliyojipangia.
- Kutathmini iwapo yale aliyopanga na kutekeleza yamemwezesha kuondokana na hali duni aliyokunayo kwenda hali nzuri zaidi.(Kufikia Hali ya Matamanio)

NB: Kama hajafikia Matamanio yake anapanga/ kutekeleza/kutathmini tena mara kwa mara au Anabadilisha Mkakati hadi atakapo fikia hali yake ya Matamanio.

Kwa njia ya Uwezeshaji, Mtu anakuwa na uwezo wa kubadili maisha yake au ya Jamii anamoishi kwa kushirikiana na wenzake. Jamii yenye Ufahamu wa hali yao, yenye Uwezo wa Kuchambua, Kupanga na Kutekeleza Mikakati yao pia inakuwa na uwezo wa kuunda Mitandao na kuwezesha kusikika hata nje ya mipaka ya Jamii yao.

Mfano : Miradi ya kijiji kuingizwa katika Mpangowa Wilaya wa Miaka Mitatu

**FAIDA** : Matokeo ni endelevu au ya kudumu kwani ni ya mtu mwenyewe.

**HASARA** : Ni mbinu inayochukua muda mrefu kabla ya kupata matokeo.

**HALI MAKANISANI:**

Mfano : AICT Dayosisi ya Pwani :

Je Mahitaji ya Kanisa yanatimizwa namna gani? Eg ujenzi ? Wageni ? Watumishi ? :

**Uliza Kanisa lenye Mradi unaozalisha fedha kwa Mahitaji yake >>>**

- Rasilmali ya Kanisa ni Waumini **Waliomo** na wale **Watakaojiunga** hapo baadaya.
- Wanaojiunga wanatoka wapi?/Tunapata vipi Waumini zaidi? (wanaoamini, watoto wanaohamia)
-

**MUUNDO WA KANISA - AICT DAYOSISI YA PWANI .**

**(Angalia Bango Kitita)**

Kutokana na Muundo huu Viongozi wa Kanisa ni Akina nani ?

Askofu/Katibu Mkuu.

Wachungaji, Wainjilist, Wazee wa Kanisa, Viongozi wa Idara. Mbalimbali.

**KUBAINISHA MAKUNDI YALIYOMO KANISANI**

- **Kanuni ya "PIGA HATUA"**

**Lengo la Kanuni hii :** Kuliwezesha Kanisa na Jamii kutambua makundi tofauti yaliyomo Makanisani na kuibua matatizo yaliyomo ili kuwa na Ufahamu wa Watu wanaowaongoza ili kuwa chachu ya Mabadiliko katika suala la Maendeleo.

**Sifa za Washiriki wa Mchezo:**

i) Mfanya biashara maarufu na mkewe, ana watoto watatu ana duka na magari ya kusafirisha watu katika miji mkubwa.
ii) Mfugaji wa ng'ombe, ana ng'ombe mia mbili, ana mke, watoto kumi na hulima kwa kutumia tracto
iii) Mwalimu wa kike wa Shule ya Msingi, mumewe hana ajira na ana watoto wanane.
iv) Mfanya kazi katika Benki kubwa, amepewa gari na nyumba ya shirika, ana watoto watatu shule za msingi.
v) Mzee wa Kanisa mwenye mke anayefanya shughuli za nyumbani, watoto wane wa kwake, na watoto yatima wawili anaowalea pamoja na mama yake mzee sana anayemtegemea na ni mgonjwa mgonjwa .
vi) Mama Mjane mwenye watoto sita wenye umri wa kwenda shule, anaishi katika nyumba ndogo, na ni mkulima mdogo.
vii) Mfanya kazi wa serikali mstaafu mzee na mkewe, wanao watoto wanaoishi Dar Es Salaa lakini hawampi msaada wowote, ana wajukuu wawili yatima waliofikia umri wa kwenda shule.

**Uwezeshaji :**

Kila mchezaji anapiga hatua moja, kama ana uwezo wa kufanya kitendo kilichotajwa, kama hawezi inabidi abaki amesimama pale alipo. Vitendo ni :

- Kama unaweza kuwapeleka watoto wako wote shule ya msingi.
- Kama unaweza kuwapeleka watoto wako wote shule za secondary.
- Unaweza kuwalipia watoto wako wote Secondary Binafsi.

- Unaweza kuajiri mtu kukuchotea maji.
- Unaweza kununua kiwanja na kujenga nyumba mjini .
- Unaweza kulipia matibabu ya familia yako.
- Unaweza kufanya urafiki na watu maarufu.
- Unaweza kununua baiskeli ya kukusaidia usafiri.
- Unaweza kununua gari ukipenda
- Unaweza kuilisha familia yako milo miwili kwa siku.

Watazamaji waangalie kama washiriki wa mchezo wanapiga hatua kulingana na uwezo wao. Baada ya mchezo kila mchezaji abaki amesimama pale alipofikia. Wachezaji wanataonekana kuwa katika makundi kadhaa.

**Maswali yanayofuatia:**

i) Waliopiga hatua nyingi zaidi ni wangapi? Akina nani?
ii) * Ni mambo gani yamechangia wewe kuwa mbele?
iii) Waliopiga hatua chache kuliko wengine ni wangapi. Wataje
iv) * Unajisikiaje kuwa nyuma ? Ni mambo gani yamechangia wewe kuwa nyuma ?
v) Una maoni gani kuhusu hali yako hiyo ?
vi) Kwa maoni yako walio mbele wanawezaje kukusaidia ?
vii) Kikundi kilichotokea kuwa cha kati ni wangapi? Wataje.?
viii) Je katika kanisa matabaka yapo? (walio mbele, kati, nyuma) Yanaletwa na nini au yanasababishwa na nini ?

**HITIMISHO :**

Kama Viongozi Kanuni hii inatusaidia :

- Kujua Makundi yaliyomo katika jamii.
- Kujua makundi yasiyojiweza katika jamii .Yataje - wajane, yatima, wazee.
- Kujua uwezo uliomo katika jamii. (ambapo wenye uwezo mkubwa watiwe moyo kuchanga zaidi wakati wenye uwezo mdogo watiwe moyo kutoa kadri ya uwezo wao).

- Kundi lipi ndiyo mhimili wa Kanisa ( wachaceh walio juu ? au wengi walio chini na kati?)

- Kanisa linawezaje kuweka Mikakati ya kuhakikisha kuwa makundi yote yanaendelea kuwa rasilmali muhimu ? Jadili : Wajane, Yatima, Watoto, Watoto Yatima, Wenye uwezo wa Uchumi mdogo.

**WAJIBU WA VIONGOZO WA KANISA**

Iwapo Waumini ndiyo rasilmali Kuu ya kanisa :,

- Je, kuna umuhimu kwa Viongozi wa Kanisa kuhakikisha kuwa Rasilmali iliyomo Kanisa inakaa/haipotei?
- 

Viongozi wahusike vipi na Vijana na Watoto ili watiwe moyo na kulelewa ili wakulie na kudumu katika kanisa za wazazi wao?

**Taja Hatua za Kuchukua :**

Sunday school?  Makundi ya vijana? Makundi maalum maalum?

Sifa za Viongozi - 2 Kor 2:14 - 15